TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)
(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)
S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamiii:instagram/fb, taro.tz
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo, Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam
"Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote"

Ref.No: Taro /P/2022/ A03 Date: 5th February 2022

# MTAZAMO WA KISHERIA KUHUSU UKUSANYAJI, UGAWAJI NA MAKATO KATIKA MIRABAHA YAWASANII WA MUZIKI TANZANIA

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** au kwa lugha ya Kiswahili **"TAASISI YA HAKI ZA WASANII"** ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiriwa na sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali iitwayo **"Non Governmental Organization Act.No.24. of 2002"**, Mnamo tarehe **26/11/2021**. Lengo kuu la **TARO** ni kuiwezesha jamii ya kitanzania kushiriki kikamilifu katika kupambana na umasikini kwa kutumia sanaa na fasihi. Katika kuakikisha inafanikiwa kwenye lengo lake kuu tajwa, moja ya shughuli za TARO ni kusaidia kulinda haki na maslahi ya wasanii wote kuhusiana na kazi zao za sanaa.

Mnamo tarehe 28 Januari 2022, kulifanyika Uzinduzi wa Tuzo za Muziki Tanzania. Shughuli hiyo ilibarikiwa na uwepo wa wadau mbalimbali wa muziki wakiwemo wasanii mbalimbali wa muziki. Katika uzinduzi huo Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COPYRIGHT SOCIETY OF TANZANIA-COSOTA) walitoa taarifa mbalimbali kuhusu ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa wasanii wa muziki, pia wakaenda mbele zaidi kwa kuwatangaza baadhi ya wasanii waliopokea mirabaha na kiasi cha fedha walichopata. Baada ya zoezi hilo kumetokea maswali mengi baina ya wasanii kuhusu uhalali wa mchakato ule. Andiko hili limejikita katika kuchambua sheria zinazoongoza mchakato mzima wa ukusanyaji wa mirabaha, ugawaji wa mirahaba na makato yanayofanywa na COSOTA kwa wasanii wa muziki katika Mirabaha.

**NUKUU**

Kutokana na barua **ya COSOTA** kwa Umma ya **tarehe 31/01/2022**, iliyoandaliwa na *Afisa elimu na Uhusiano* **(Anitha Jonas),** inaeleza kuwa "..Fedha za mirabaha zimekusanywa kutoka katika maeneo mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, Baa, Kumbi za starehe, Hoteli na Vyombo vya usafiri".

Kwa mujibu wa **Afisa Mtendaji Mkuu (COSOTA)**, Mnamo tarehe **28 Januari 2022**, katika Uzinduzi wa Tuzo za Muziki Tanzania alihutubia kwa kusema *" Tumefanya **sampling** na tumeweza kugawa jumla ya shilingi 312,290,259/=………"*

## SAMPLING NI NINI?

Kwa mujibu wa **kifungu cha 3** cha sheria ya takwimu iitwayo **The Statistics Act (CAP. 351. R.E 2019),** kimeelezea maana ya neno **sampling** . Kwa lugha nyepesi SAMPULI ni kuchukua taarifa za vitu vichache vinavyohusiana na vitu vingi kuwakilisha vitu vingi. Mfano kuwahoji watu 10 wa wilaya ya kinondoni, kisha taarifa utakazozipata zitumike kuwakilisha watu wote wa wilaya ya Kinondoni.

## HOJA ZA KISHERIA

**Je COSOTA wametumia utaratibu sahihi kukusanya mirabaha ya kazi za muziki?**

**A.** Sheria iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002)** katika kifungu cha **47** kifungu kidogo **(a)** kimeipa **COSOTA** mamlaka ya kukusanya na kugawa mirabaha na mapato mengine yoyote yanayoweza kupatikana kutokana na haki za wabunifu kama zilivyoorodheshwa na sheria hiyo.

**B.** Kanuni ziitwazo **The Copyright (Licensing of Public Performances and Broadcasting) Regulations, 2003.GN.NO.328 0F 2003** zimeelekeza COSOTA kukusanya mirabaha kwenye Bar, clubs, hotels, Restaurants, Airports, saloons, coffee shops, Meli, Pubs, viwanja vya ndege, Vyombo vya habari nakadharika kwa kuzingatia masharti yafuatayo:-

i. Ni marufu kwa mtu yoyote kupiga kazi za muziki kwenye umma au kuzirusha kwenye vyombo vya habari bila kupata leseni ya COSOTA. **Rejea kanuni ya 3**

ii. COSOTA wanatakiwa kuwapa leseni wanaopiga kazi za muziki kwenye umma au kuzirusha kwenye vyombo vya habari kwa kutumia fomu maalum. Hao watakaopewa leseni wanatakiwa kulipa ada na ushuru kama ilivyooanishwa kwenye **jedwali la pili la kanuni**. **Rejea kanuni ya 5(1)(b)**

**Jedwali la pili la kanuni** linatambua mirabaha kwa mfumo wa ada na ushuru. Jedwali hilo ndio linaelekeza eneo husika lilipe ada kiasi gani na ushuru kiasi gani kwa matumizi ya kazi za muziki. Katika sehemu zote ambazo ushuru na ada zinakusanywa, ni katika vyombo vya habari pekee, kanuni zimeagiza kuwe na log sheet yaani mfumo wa kujua nyimbo ipi imepigwa na imepigwa mara ngapi. **HIVYO BASI katika kanuni hizi,** ukitoa vyombo vya habari, sehemu zote zilizobaki mapato yanakusanywa bila kujua yanaihusu kazi ipi ya muziki.

**C.** Kwa mujibu wa Jedwali la Tatu, kipengele cha **2 (a)** ya kanuni ziitwazo **Copyright and Neighbouring rights (Copyrighted Works-Communication to the public) Regulations 2015. GN.NO.29 OF 2016** inaelekeza COSOTA kukusanyaji wa mirabaha kwenye makampuni ya mawasiliano, Dijitali/huduma za mtandaoni na kurasa za mtandaoni. Utaratibu wa kukusanya unatumia log sheet. **LOG SHEET** ni fomu

TAZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

inayojazwa na watumiaji kazi za muziki kuweka kumbukumbu lini nyimbo ilipigwa na ilipigwa mara ngapi.

**Je ni utaratibu gani unatumika kugawa mirabaha ya kazi za muziki kwa wahusika?**

**A.** Kwa mujibu wa **kanuni ya 8** ya kanuni ziitwazo **The Copyright (Licensing of Public Performances and Broadcasting) Regulations, 2003.GN.NO.328 0F 2003** zinaagiza kwamba, COSOTA kwa kufuata taratibu zao, wanapaswa kulipa mirabaha au mapato mengine yaliyopatikana, kwenda kwa **mtu anaestahili (person entitled thereto)** kwa kutumia makusanyo ya ada walizokusanya kwa kuzingatia masharti ya **Jedwali La Tatu La Kanuni hizi. HIVYO BASI,** anaelipwa lazima awe anastahili kulipwa na ulipaji lazima ufuate masharti ya kanuni. Jedwali hilo limekua kimya au kwa lugha nyingine limeacha au limeruka kuelezea utaratibu wa ugawaji wa mirabaha kwenye makusanyo ya ada na ushuru kwenye vyanzo vingine nje ya vyombo vya habari.

**B.** Kwa mujibu wa Jedwali la tatu, kipengele cha **2(3)** na **(4)** cha kanuni ziitwazo **The Copyright (Licensing of Public Performances and Broadcasting) Regulations, 2003.GN.NO.328 0F 2003** inaitaka COSOTA itumie log sheet katika kugawa mirabaha inayotoka katika vyombo vya habari **.** Kanuni hazijaongelea ugawaji wa marabaha kutoka kwenye vyanzo vingine.

**C.** Kwa mujibu wa **kanuni ya 12** ya kanuni ziitwazo **Copyright and Neighbouring rights (Copyrighted Works-Communication to the public) Regulations 2015. GN.NO.29 OF 2016** inaagiza kwamba, COSOTA kwa kutumia taratibu zilizoainisha katika **Jedwali La Tatu La Kanuni** , wanapaswa kulipa mirabaha au mapato mengine yaliyopatikana kwenda kwa **mtu anaestahili (person entitled thereto)** kwa kutumia makusanyo ya ada walizokusanya kupitia kanuni hizi**.**

**D.** Kwa mujibu wa Jedwali la Tatu, kipengele cha **2 (c)** cha kanuni ziitwazo **Copyright and Neighbouring rights (Copyrighted Works-Communication to the public) Regulations 2015. GN.NO.29 OF 2016** inaagiza COSOTA kutumia log sheet kwenye kugawa mirabaha inayotoka katika makampuni ya mawasiliano, Dijitali/huduma za mtandaoni na kurasa za mtandaoni.

**E.** Kwa mujibu wa **kifungu cha 5** cha sheria ya takwimu iitwayo **The Statistics Act (CAP. 351. R.E 2019),** kinaeleza kuwa ili kulinda na kuwezesha uadilifu na uaminifu wa takwimu rasmi, **Ofisi ya Taifa ya Takwimu** inatakiwa kuhusika katika uandaaji wa takwimu rasmi. Sheria hiyo hiyo katika **kifungu cha 6,** imeoanisha majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuwa:-

i. Kuishauri serikali na umma kwa ujumla kuhusiana na maswala yote ya takwimu
ii. Kutoa takwimu kwa wakati, zenye ubora wa hali ya juu na zinazoweza kutegemewa
iii. Kuratibu takwimu rasmi

TAZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION TARO

iv. Kuratibu na kusimamia mfumo wa takwimu wa nchi

**Je kuna uhalali wa kisheria kwa COSOTA kufanya makato katika mirabaha ya wasanii?**

A. Sheria iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002)** katika kifungu cha **48** kifungu kidogo **(a)** kimeeleza kuwa moja ya vyanzo vya mapato vya COSOTA ni ***ada zote zitakazolipwa kutokana na sheria hii***. Sheria imetumia maneno ***"all fees payable under this act".***Sheria iko wazi ni ada zitakazolipwa na wanachama sio zitakazokatwa kutoka katika mirabaha ya wanachama.

**B.** Kwa mujibu wa kanuni zinazoongoza usajili wa wanachama na kazi zao COSOTA, ziitwazo **The Copyright And Neighbouring Rights (Registration Of Members And Their Works) Regulations**, **2005. GN. NO.6 OF 20 January 2006**, na marekebisho yake yaani **The Copyright And Neighbouring Rights (Registration Of Members And Their Works) Regulations**, **2013 GN.NO.413 OF 2013, katika kanuni ya 5,** zinaelekeza kuwa ada zote zinazohusiana na maombi ya uanachama na ada za kila mwaka, zinatakiwa ziwe ada kama zilivyoainishwa na Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi na zinaweza kubadilika mara kwa mara kama itavyoelekezwa na bunge. **Kanuni hizi hazijaielekeza popote, COSOTA kukata mirabaha ya wanachama kwa lengo la kulipa ada za mwaka za uanachama.**

**C.** Kwa mujibu wa kanuni ziitwazo **The Copyright (Licensing of Public Performances and Broadcasting) Regulations, 2003.GN.NO.328 0F 2003** zimeelekeza COSOTA kufanya makato yafuatayo katika mirabaha iliyokusanywa maeneo yote kasoro kwenye makampuni ya mawasiliano, Dijitali/huduma za mtandaoni na kurasa za mtandaoni :-
( Rejea Jedwali la Tatu , kipengele 5**(1)(a) na (b)** cha kanuni hii)

i. COSOTA kukata kiasi kisichozidi asilimia 30% ya makusanyo yote ya mirabaha kwa ajili ya kusaidia gharama za uendeshaji wa taasisi

ii. Baada ya kukata kiasi tajwa hapo juu (kipengele **i**), Asilimia 10% ya mirabaha iliyopatikana kutoka katika haki za mbunifu kwenye uandishi wa kazi za muziki na maigizo inatakiwa kulipwa kwenda kwenye **MFUKO WA JAMII NA UTAMADUNI** wa mbunifu aliye mwanachama.

iii. Asilimia 5% mirabaha iliyopatikana katika haki za muimbaji na mtayarishaji wa kazi ya muziki kupitia log sheet inatakaiwa kulipwa kwenda **MFUKO WA JAMII NA UTAMADUNI** wa mbunifu aliye mwanachama COSOTA. **Kanuni hizi hazijaielekeza popote, COSOTA kukata mirabaha ya wanachama kwa lengo la kulipa ada za mwaka za uanachama.** Kanuni zinaelekeza kuwa makusanyo ya mirabaha kutoka katika **mifuko** yanaweza kutumiwa na COSOTA kwa maamuzi ya Bodi yao, baada ya kuruhusiwa na bunge.

**D.** Kwa mujibu wa kanuni ziitwazo **Copyright and Neighbouring rights (Copyrighted Works-Communication to the public) Regulations 2015. GN.NO.29 OF 2016** zimeielekeza COSOTA kufanya makato yafuatayo katika mirabaha iliyokusanywa

kwenye makampuni ya mawasiliano, Dijitali/huduma za mtandaoni na kurasa za mtandao ni :- ( Rejea Jedwali la Tatu , kipengele **5** cha kanuni)

i. COSOTA kukata kiasi kisichozidi asilimia 30% ya makusanyo yote ya mirabaha kwa ajili ya kusaidia gharama za uendeshaji wa taasisi

ii. Baada ya kukata kiasi tajwa hapo juu (kipengele **i**), Asilimia 10% ya mirabaha iliyopatikana kutoka katika haki za mbunifu kwenye uandishi wa kazi za muziki na maigizo inatakiwa kulipwa kwenda kwenye MFUKO WA JAMII NA UTAMADUNI wa mbunifu aliye mwanachama .

**iii.** Asilimia 5% mirabaha iliyopatikana katika haki za muimbaji na mtayarishaji wa kazi ya muziki kupitia log sheet inatakaiwa kulipwa kwenda MFUKO WA JAMII NA UTAMADUNI wa mbunifu aliye mwanachama COSOTA.

**<u>HITIMISHO</u>**

Ukusanyaji wa mirabaha uliofanywa na COSOTA uliacha kukusanya mirabaha kwenye makampuni ya mawasiliano, Dijitali/huduma za mtandaoni na kurasa za mtandaoni , ambapo sheria imeweka matumizi ya log sheet. Kwenye vyanzo hivyo ukusanyaji wa mirabaha una miongozo inayoeleweka kama kwenye vyombo vya habari. COSOTA wamekusanya ada(mapato) kutoka katika  Baa, Kumbi za starehe, Hoteli na Vyombo vya usafiri bila kujua nyimbo zinazohusiana na mapato yale/ wanaostahili kupata malipo kutokana na mapato yale.

Kanuni zote zinazopatika kwenye sheria ya Hakimiliki,  zimeagiza wazi kuwa ugawaji wa mirabaha ufanywe kwa watu wanaostahili kupata mirabaha kwa kufuata masharti ya kanuni.Ugawaji wa mirabaha uliofanywa na COSOTA umehusisha ugawaji wa mirabaha kwa wasanii wasiostahili kutoka kwenye makusanyo yasiyo na log sheet. Pia COSOTA wamegawa mirabaha kwa kutumia utaratibu ambao haujaoanishwa na sheria. Kanuni hazijaelekeza matumizi ya **Sampling** katika kugawa mirabaha kwa wasanii .Lakini COSOTA wametumia **sampling**. Sampling ni sehemu ya Takwimu, COSOTA hawaruhusiwi kisheria kufanya kazi yoyote inayohusiana na takwimu**.** Kwa mujibu wa sheria**,** **Ofisi ya Taifa ya Takwimu** pekee ndio yenye mamlaka ya kufanya takwimu na ndio yenye kuaminika nchini..

Sheria mama ya hakimiliki na kanuni zake zote, hazijaielekeza popote, COSOTA kukata mirabaha ya wanachama (**Deduction of Royalties)** ili kupata ada kama chanzo cha mapato ya COSOTA. Lakini sheria inatambua malipo ya ada kutoka kwa wanachama **(Fee payable)**  kama chanzo cha mapato ya COSOTA.

ASANTENI
MUNGU AIBARIKI TANZANIA
MUNGU ATUBARIKI WATANZANIA
(Kazi iendelee)

Wako Mtiifu

**Mkurugenzi Mkuu wa Utawala**
**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**